# TNMC Habari

Toleo No. 0018

TOLEO MAALUMU Februari, 2025

HALIUZWI www.tnmc.go.tz @tnmchabari

# Watumishi TNMC Waketi kwa Kikao Dodoma

Habari Uk. 01





**Rais Samia Apokea Tuzo Maalumu ya Kimataifa "The Global Goalkeeper Award".**

Ukurasa 2




**Wauguzi, wakunga watakiwa kuhuisha Leseni Za kitaaluma Zilizokwisha Muda Wake**

Ukurasa 4



**wahudumu Watoa Huduma Chumba Cha Upasuaji Maweni RRH Wanufaika Na Mafunzo Kutoka TNMC.**

Ukurasa 7



TNMC 22nd Anniversary

Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania ni Mamlakaya Kisheria inayosimamia wanataaluma na taaluma za Uuguzi na Ukunga Tanzania chini ya Sheria ya Mwaka 2010 na kanuni zake (The Nursing and Midwifery Act, 2010) ili kuhakikisha huduma zinazotolewa na wauguzi na wakunga nchini Tanzania ni za kiwango kinachokubalika na salama kwa jamii.

# TIMU YA WAHARIRI

**MWENYEKITI**

**Bi. Agnes Mtawa**

**MHARIRI**

**Mwakapiso Ndimmyake**

**WARATIBU**

**Irene Chilewa**
**Rose Mhando**

**MSANIFU JARIDA**

**Ezekiel Nyalusi**

# Watumishi TNMC Waketi kwa Kikao kazi Dodoma



Na. Ezekiel Nyalusi

Watumishi wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania wameketi siku mbili katika katika kikao cha watumishi kilichoongozwa na mwenyekiti ambaye ni Msajili Bi. Agnes Mtawa, ambapo zaidi ya watumishi 50 wanashiriki kikao, kilichofanyika Jijini Dodoma kwa lengo la kujadili masuala mbalimbali ya kiutumishi.

Miongoni mwa masuala yaliyojadiliwa bajeti ya tasisi kwa mwaka wa fedha 2025/26 ambapo Mchumi wa Taasisi Bw. Filemon Mlageli aliwasilishavipaombele vya bajeti hiyo.

***"katika mwaka wa fedha 2025/26 vipaombele vya taasisi vimezingatia masuala mtambuka (Cross-cutting Objectives A, B, Y na X ) lengo ni Kuimarisha upatikanaji wa huduma bora za Afya zinazotolewa na vituo vya kutolea huduma za Afya kuanzia ngazi ya zahanati hadi Taifa na kuandaa pamoja na kusimamia mkakati wa maadili kwa wauguzi na wakunga Tanzania kwalengo la Kusimamia utoaji wa huduma staha zenye heshima kwa wananchi katika ngazi zote za utoaji wa huduma"*** -alisema Bw. Filemoni

Naye, Bi. Zainabu Bakari ambaye ni Afisa Elimu na Mafunzo kutoka TAKUKURU ametoa Elimu ya kupambana na Rushwa kwa wafanyakazi wa TNMC Lengo ni kukumbushana Sheria na taratibu za kupambana na kuzuia rushwa hasa maeneo ya kazi.

Kwa upande wake Bwana Thamson Tighati ambaye ni Katibu wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali na Afya Tanzania (TUGHE) Mkoa wa Manyara na Celvin Mapembe wamebainisha Majukumu ya msingi ya Chama hicho kama yalivyoainishwa katika Katiba ya Chama cha Wafanyakazi wa Serikali na Afya Tanzania (TUGHE) ya Mwaka 2006 kuwa ni kuunganisha, kuelimisha, kutetea haki, wajibu na maslahi ya wanachama kwa wakati kwa kutumia watumishi na viongozi makini, Sambamba na hilo walitoa ushauri kwa watumishi wa TNMC kujiunga na chama hicho.

Lakini pia, watumishi walifundishwa masuala ya utawala bora Mada iliyowasilishwa na Afisa kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya utumishi na utawala bora Bw. Rocky Setembo ***"kiukweli nimetembea taasisi nyingi nikitoa semina ila kwa TNMC mmenikosha hasa kwa upande wa kuzingatia uvaaji wa mavazi nadhifu hongera msajili kwa kusimamia hilo"*** alisema bwana Rocky.

Hata hivyo, Pamoja na mambo mengine Bwana Rocky alifundisha suala la Kanuni Nane (8) za Maadili ya Utendaji ambazo ni Kutoa Huduma Bora, Utii kwa serikali, Bidii ya kazi, Kutoa huduma bila upendeleo,Kufanya kazi kwa uadilifu, Kuwajibika kwa umma,Kuheshimu sheria na Matumizi sahihi ya taarifa.

Kwa muda wa siku mbili za kikao watumishi walipata fursa za kupima Afya zao ikiwa ni pamoja na shinikizo la Damu, UKIMWI na kisukari.

# Rais Samia ApokeaTuzo Maalum Ya Kimataifa Ya “The Global Goalkeeper Award”.



Na. Mwandishi Wetu.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amepokea Tuzo Maalum ya Kimataifa ya The Global Goalkeeper Award kutoka kwa Rais wa Kitengo cha Usawa wa Jinsia Taasisi ya Gates, Dkt. Anita Zaidi, kwenye hafla iliyofanyika katika Hoteli ya Hyatt Regency Jijini Dar es Salaam tarehe 04 Februari, 2025.

Tuzo hiyo hutolewa kwa viongozi waliowezesha nchi zao kuharakisha maendeleo kuelekea kufikia malengo ya maendeleo endelevu, Mhe. Rais Samia amepewa Tuzo hiyo katika kipengele cha mapambano dhidi ya vifo vya wajawazito na watoto wachanga chini ya umri wa miaka mitano.

*“Nilipochukua madaraka, niliahidi kwamba pamoja na kuwekeza katika vituo vya Afya na wafanyakazi wa sekta ya Afya, tutaipa kipaumbele Afya ya Mama na Mtoto. Tangu mwaka 2021, tumetekeleza hatua mbalimbali za kuboresha Afya ya uzazi, Afya ya Mama, watoto wachanga, vijana, pamoja na lishe.”* Rais Samia Suluhu akipokea Tuzo ya Gates Goalkeeper Award.

Rais Samia amesema kuwa tuzo hiyo inatia moyo, kuona kwamba mikakati mbalimbali iliyotekelezwa imechangia kupunguza kiwango cha vifo vya akinamama wajawazito pamoja na vifo vya watoto wachanga chini ya miaka mitano.

Vifo vya wajawazito vimepungua kutoka vifo 556 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2020 hadi vifo 104 kwa kila vizazi hai 100,00 hadi hivi sasa huku vifo vya watoto wenye umri chini ya miaka mitano vimepungua kutoka vifo 67 kwa kila vizazi hai 1,000 mwaka 2020 hadi vifo 43 kwa kila vizazi hai 1,000 hadi hivi sasa.

# Wataalamu wa Afya watakiwa kujenga Ushirikiano Wa Utoaji Huduma Bora Za Afya



Waziri wa Afya Mhe. Jenista Mhagama amewataka wataalamu pamoja na wadau wa Sekta ya Afya kushirikiana katika kuanzisha kituo cha ubunifu wa utoaji huduma bora za Afya ya Mama na Mtoto nchini.

Waziri Mhagama ametoa maagizo hayo Februari 06, 2025 alipokutana na wawakilishi kutoka katika Hospitali ya Kilutheri ya Haydom, Manyara na kujadiliana kuhusu ushirikiano zaidi wa utoaji wa huduma za Afya ya uzazi, Mama na Mtoto.

***"Upo umuhimu wa kuanzisha kituo cha umahiri wa utoaji wa huduma bora za Afya ya uzazi Mama na Mtoto, tunataka kuwa na kituo ambacho kitatoa fursa kwa wataalamu kubuni njia bora za kuboresha huduma za Afya ya uzazi ikiwa ni pamoja na matumizi ya teknolojia za kisasa za kufuatilia Afya ya Mama na Mtoto,"*** amefafanua Waziri Mhagama.



Amesema kituo hicho pia kitakuwa jukwaa la kuanzisha miradi ya elimu kuhusu lishe bora, huduma za uzazi na uangalizi wa watoto wachanga ambapo lengo kuu likiwa ni kuhakikisha kuwa huduma hizi zinapatikana kwa urahisi na zenye ubora kwa familia katika maeneo yote nchini.



Waziri Mhagama amesema kuwa, Serikali imepiga hatua katika kupunguza vifo vya Mama na Mtoto kwa kuanzisha mikakati madhubuti ya kuboresha huduma za Afya katika ngazi zote ikiwemo uwekezaji katika miundombinu ya Afya, upatikanaji wa huduma za uzazi pamoja na mafunzo kwa wahudumu wa Afya.

Hata hivyo amesema bado mbinu mpya pamoja na mikakati endelevu ya uboreshaji huduma za Afya ya uzazi zinahitajika zaidi ili kuboresha huduma za afya ya uzazi, Mama na Mtoto.

Kwa upande wake Dkt. Paschal Mdoe, kutoka Hospitali ya Haydom amesema wataendelea kushirikiana na Serikali katika utoaji wa huduma bora za Afya ikiwemo masuala ya Afya ya uzazi Mama na Mtoto ili wananchi waendelee kupata huduma bora.

# Wauguzi, wakunga watakiwa kuhuisha Leseni Za kitaaluma Zilizokwisha Muda Wake



Na. Ezekiel Nyalusi

Wauguzi na wakunga wote nchini wanakumbushwa kuhuisha leseni zao zilizokwisha muda wake tangu mwezi Disemba 2024, kwani kuendelea kutoa huduma pasipokuwa na leseni hai ni kosa kisheria kwa mujibu wa Kifungu cha 38(i) (a) (b) cha Sheria ya Uuguzi na Ukunga.

Wito huo umetolewa na Mkurugenzi wa Usajili, leseni na Maadili TNMC Bi.Jane Mazigo akizungumza na TNMC HABARI tarehe 12.02.2025 jijini Dodoma.

***"Naomba nitoe wito kwa wauguzi na wakunga wote nchini ambao bado hawajahuisha leseni zao mpaka sasa wafahamu kuwa kwa mujibu wa Kifungu tajwa hapo juu, Muuguzi au Mkunga ambaye atatoa huduma pasipokuwa na leseni hai, ataondolewa kwenye daftari la usajili au kutozwa faini kwa mujibu wa Sheria"*** Alisema Bi Mazigo.

Mkurugenzi aliongeza kuwa, uhuisahaji wa leseni unakwenda sambamba na Mafunzo ya kujiendeleza kazini (CPD) ili kuboresha huduma za Uuguzi na Ukunga, waajiri wote wanakumbushwa kufanya uhakiki wa wauguzi na wakunga mliowaajiri ili wawe na leseni hai za kitaaluma.

***"Na hapa Sheria ipo wazi kuwa, waajiri kutoa ajira kwa muuguzi au mkunga asiye na leseni hai ni kosa kisheria chini ya Kifungu cha (44) cha Sheria ya Uuguzi na Ukunga ya Mwaka 2010 kwani kufanya hivyo unaweza kushitakiwa na kutozwa faini kwa mujibu wa Sheria"*** alisema Bi. Mazigo

# Madaktari Wasio Na Mipaka Watembelea Ofisi Ya Msajili TNMC Dodoma



Na. Mwandishi Wetu

Madaktari Wasio na Mipaka (MEDECINS SANS FRONTIERES- MSF) wametembelea ofisi ya Msajili wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania ili kufahamu utendaji kazi wake hususani kuhusu usajili wa wauguzi na wakunga hapa nchini wakiwa wadau mhimu katika utoaji wa huduma za kiafya hapa nchini.

## Madaktari Wasio na Mipaka (MEDECINS SANS FRONTIERES- MSF) ni akika nani?

Hili ni Shirika lisilo la kiserikali na la kimataifa linaoundwa na Madaktari na wafanyakazi wa sekta ya Afya.

Pia linapokea wafanyakazi kutoka kwenye taaluma zingine ikiwemo wauguzi na wakunga ambao wanaweza kusaidia kutimiza malengo ya shirika.

Wafanyakazi wake wote wanazingatia kuheshimu Sheria na kanuni za nchi husika.

Pamoja moja na mambo mengine MSF inatoa msaada kwa watu walio kwenye shida, walioathirika na majanga ya asili au ya kibinadamu na waathirika wa vita. MSF wanafanya hivyo bila ya ubaguzi wa rangi, dini au misimamo ya kisiasa. MSF inafanya kazi bila kuegemea upande wowote kwa mujibu wa maadili ya kitabibu na haki ya msaada wa kibinadamu, shirika hili lina uhuru wa kutosha katika kufanya kazi zake.

Hata hivyo, Wafanyakazi wa MSF wanatakiwa kuheshimu maadili ya kitaaluma na kulinda uhuru wake dhidi ya ushawishi wa kisiasa, kidini na kiuchumi. Wafanyakazi wanaweza kukabiliana na changamoto mbalimbali wawapo kwenye kazi zao na hawapaswi kuomba malipo yoyote ya fidia zaidi ya yale ambayo MSF inaweza kuwalipa.

# Watoa Huduma Chumba Cha Upasuaji Maweni RRH Wanufaika Na Mafunzo Kutoka TNMC.



Na. Mwandishi Wetu

Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania (TNMC), limetoa mafunzo elekezi kwa Madaktari, wauguzi, wakunga na wauguzi wataalamu wa dawa za usingizi na ganzi wanaofanya kazi katika vyumba vya upasuaji pamoja na baadhi ya watumishi kutoka vitengo mbalimbali vya kutolea huduma wapatao 28 katika Hospitali ya Rufaa Maweni mkoani Kigoma.

Mafunzo hayo yameongozwa na Afisa Muuguzi Mbobezi chumba cha upasuaji kutoka TNMC Bi. Salome Kassanga alifundisha namna bora ya kutoa huduma katika chumba cha Upasuaji "Theatre Management" kwa lengo la kumlinda mgonjwa kuwa salama wakati na baada ya upasuaji.

Akizungumza katika ufunguzi wa mafunzo hayo, Mwezeshaji kutoka Baraza la Uuguzi na Ukunga amesema kuwa, lengo la kutoa mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo madaktari, wauguzi, wakunga na wataalamu wengine katika chumba cha Upasuaji ili kuboresha huduma kwenye chumba cha Upasuaji na kukidhi viwango vya Kimataifa.

*"Tunatoa mafunzo haya ili kuhakikisha kuwa vyumba vya upasuaji kunakuwa na misingi bora ya usimamizi na uendeshaji, misingi ya kudhibiti maambukizi kwa wagonjwa (IPC), uzingatiaji wa Maadili, Sheria, kanuni na miongozo katika chumba cha upasuaji, uzingatiaji wa kuweka taarifa za wagonjwa wanaopatiwa huduma za upasuaji (Documentation), pamoja na kulinda usalama wa mgonjwa na watoa huduma"* alisema Bi. Kassanga.

Hata hivyo, zaidi ya watumishi 59 wa Hospitali ya mkoa wa Kigoma (Maweni RRH) wamekumbushwa juu ya utoaji wa huduma kwa kuzingatia maadili, miiko, uadilifu, ikiwa ni pamoja na uvaaji wa Sare maalumu za chumba cha upasuaji kulingana na miongozo, uzingatiaji wa kuweka taarifa sahihi za wateja wanaopatiwa huduma (Documentation), pamoja na kulinda usalama wa mgonjwa na watoa huduma.



# Tanzania ina Uwezo Mkubwa Katika Kukabilina na Dharura za Afya



Na. Ezekiel Nyalusi

Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na wadau wa Sekta ya Afya imefanya maendeleo makubwa katika kujenga uwezo wa kukabiliana na dharura za afya ikiwa ni pamoja na kuwekeza katika mifumo ya afya, kuimarisha ushirikiano na wadau, kuanzisha mifumo ya tahadhari mapema pamoja na ufuatiliaji wa abiria na vyombo vya usafiri.

Hayo yamesemwa na Waziri wa Afya Mhe. Jenista Mhagama Februali 10, 2025 wakati akitoa wasilisho katika Mkutano wa 74 wa Mawaziri wa Afya wa Jumuiya ya Afya ya Nchi za Afrika Mashariki, Kati, na Kusini (ECSA – HC) kuhusu namna ya kukabiliana na magonjwa ya mlipuko na masuala ya dharura za afya za umma katika kanda hiyo uliofanyika nchini Malawi

*"Magonjwa ya mlipuko yamekuwa yakijitokeza mara kwa mara na husababisha dharura za kiafya na kuhatarisha usalama wa afya za wananchi, Serikali ya Tanzania chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan tumefanikiwa kwa kiasi kikubwa kuweza kukabiliana na dharura za afya na kuimarisha udhibiti dhidi ya magonjwa ya mlipuko,"* amesema Waziri Mhagama.

Waziri Mhagama amesema mnamo mwezi Machi mwaka 2023 , Tanzania ilikumbwa na mlipuko wa ugonjwa wa Marburg kwa mara ya kwanza na ilifanikiwa kudhibiti ndani ya miezi mitatu, lakini pia hivi karibuni mlipuko wa pili ulitokea na hatua zote za kudhibiti zilitekelezwa haraka na Tanzania ina uwezo wa kudhibiti mlipuko huo pia.

Vile vile, Waziri Mhagama ameweka wazi juu ya umuhimu wa kupitisha suluhu endelevu za uzalishaji wa huduma za chanjo, tiba pamoja na bidhaa za matibabu ili kukabiliana na tishio la afya ikiwemo magonjwa ya milipuko.

Waziri Mhagama ameuambia mkutano huo kuwa Tanzania itaendeleza ushirikiano na Jumuiya ya Afya ya ECSA katika juhudi za usalama wa afya wa Kikanda na Kimataifa ambapo ameiomba Jumuiya hiyo kuendelea kushirikiana na Tanzania hasa katika kusaidia uratibu wa Chuo cha Madaktari wa Afya ya Umma (ECSA-COPHP).



JARIDA LA BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA

Limeandaliwa na Kitengo cha Uhusiano
Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania
S.L.P 1736 DODOMA , **Simu: 0736 00 60 60**
Barua Pepe:Info@tnmc.go.tz
Tovuti:www.tnmc.go.tz

HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA